ANGLOGOLD ASHANTI

Watu ndio Ubia ...
Ubia Wetu ni Watu.

Ninaishi kwa falsafa rahisi ya uongozi: **Ubia huu ni wetu tunaousimamia... na mustakabali utaundwa na sisi"**. Tukichukulia usemi huu kama sehemu ya kuanzia, jambo la muhimu kufahamu kuhusu ubia wetu ni kuwa sio juu ya wingi wa hifadhi ya dhahabu, au kinu cha kuchechua dhahabu, wala kofia za kujikinga tu, bali kiini cha yote ni watu: **Watu ndio Ubia...Ubia wetu ni Watu**

Sisi ni watu ambao kila mmoja ana matazamio, malengo, na mitizamo yake juu ya maisha, na kila mmoja wetu anatoka katika historia ya kipekee. Ili kuweza kuunda mustakabali wa pamoja kama ubia wenye mafanikio, tunapaswa kumuonyesha kila mmoja wetu heshima na utu. Lazima tulenge katika kujenga uhusiano utakayomuwezesha kila mmoja wetu aweze kutoa mchango wake katika mafanikio yetu ya pamoja, uhusiano uliojengwa katika misingi ya uaminifu wa dhati. Na hii ndio sababu, usalama ndio tunu yetu ya awali, kwa kuwa kila mmoja wetu ana thamani. Ni jukumu binafsi la kila mmoja wetu na letu sote kujenga mazingira kufanyia kazi yaliyo salama na yanayodumisha afya, yasiyosababisha madhara wala magonjwa.

Kijitabu hiki kinahusu Dhima, Dira, Tunu na Mikakati tunayojenga. **Huu ndio mwanzo wa kuungana pamoja kuujenga mustakabali wetu.** Ili kuunda mafanikio yetu ya pamoja, hatuna budi kuyaishi maneno yaliyo katika kijitabu hiki na kuyapa maana ili kwa pamoja tuweze **kujenga njia ya kuelekea katika uundaji wa maadili ubia wetu... njia iliyojengwa na kikundi cha walio na kiu ya ushindi.**

Mark Cutifani
Afisa Mwendeshaji Mkuu

Dira Yetu

"Kuwa Kampuni Kinara ya Uchimbaji"

Dhima Yetu

“Tunaunda thamani kwa ajili ya wanahisa wetu, wafanyakazi wetu na washirika wetu wa kibiashara na kijamii kwa kuzingatia usalama na uwajibikaji katika kutafiti, kuchimba na kuuza mazao ya kazi yetu. Kitovu chetu ni dhahabu na tutaendelea kijihimu kwa kutengeneza fursa za uchimbaji wa madini mengine pale ambapo tunawaweza kuongeza rasilimali, ujuzi na uzoefu wetu ili kudumisha mafanikio yetu”

Tunu Zetu

Watu ndio Ubia Wetu ...

Usalama ndio tunu yetu ya awali.

Tumeweka watu awali ya yote na hivyo tumeweka kipaumbele katika utendaji na mifumo ya kazi inayozingatia usalama na afya. Tunawajibika kubuni mbinu mpya na za kisasa ili kuhahakikisha kuwa katika maeneo yetu ya kazi hakuna kuumia wala kuugua kunakotokana na utendaji wa kazi. Tunaiishi kila siku mpya kwa ajili ya kila mmoja wetu na kutumia utashi, vipawa, raslimali na mifumo yetu ili kwa pamoja kutimiza nia yetu kuu.... Yaani Kujali.

Tunajali Utu na Heshima Ya Kila Mmoja.

Tunaamini kuwa watu wanaoheshimiwa na kuaminishwa majukumu, hurudisha fadhila kwa kuonyesha utendaji wa hali ya juu. Tunajihimu kulinda utu wa watu, uhuru wao binafsi katika mahusiano yetu yote, tukiheshimu thamani yao binafsi, tukiwaheshimu jinsi walivo, na kuthamini mchango wa kipekee wanaoweza kuutoa katika kufanikiwa kwa biashara yetu. Sisi ni wakweli miongoni mwetu wenyewe na kwa wengine, na tunahusiana na washirika wetu wa kibiashara na kijamii kwa kuzingatia maadili mema.

Tunathamini Tofauti Zilizo Miongoni Mwetu.

Tunalenga kuwa vinara ulimwenguni kote tukiwa na watu sahihi katika nafasi sahihi. Tunahimiza mchanganyiko na umoja katika kazi, tukivuna matunda ya utajiri unaopatikana kutoka mchanganyiko w tamaduni, fikra, uzoefu na ujuzi tofauti ambao kila mfanyakazi analeta katika biashara yetu.

... Ubia Wetu ni Watu.

Tunawajibika kwa matendo yetu na Kujitahidi kutimiza ahadi zetu.

Tunalenga kutimiza malengo na hivyo tunatenda yale tunayosema kuwa tunafanya. Tunabeba dhamana na kuwajibika kwa shughuli zetu, mienendo yetu, maadili yetu na vitendo vyetu. Tunalenga kuwa na kiwango cha juu kabisa kiutendaji tunapotekeleza kazi zetu na hivyo kuendelea kuhakikisha tunatimiza wajibu wetu kwa wenzetu, washirika wa kibiashara na kijamii, na wanahisa wetu.

Jumuiya na Jamii tunamoendesha shughuli zetu zitakuwa na hali bora zaidi kwa uwepo wa AngloGold Ashant mahali hapo.

Tunadumisha na kuhimiza haki za msingi za binadamu mahali tunapoendesha biashara. Tunashiriki katika ujenzi wa ubia kwa misingi ya heshima na manufaa ya pande zote katika jamii tunamofanya kazi. Tunalenga kuzirithisha jamii wenyeji wetu mustakabali endelevu.

Tunasheshimu Mazingira.

Tumejidhatiti kuendelea kuboresha mchakato wa utendaji wetu kila wakati ili kuzuia uchafuzi wa mazingira, kupunguza taka chafu, kungeza ufanisi katika matumizi ya kemikali za asili na kuwa na tija katika matumizi maliasili. Tutabuni mbinu za kisasa kupunguza athari kwa mazingira na hali ya hewa.

Ili Kuweza Kuyafikia Malengo Ya Ubia Wetu Tumejikita Katika Mikakati Mitano Mikuu

1. Watu Ndio Ubia Wetu
Tunao mchakato mzuri wa uongozi na usimamizi ili kujenga mazingira ambamo kila mmoja atakuwa na utashi wa kujitoa kwa uwezo wake wote.

2. Kupanua Wigo
Mafanikio yetu katika kuvumbua madini na miradi inayolenga kupanuka ndio mhimili muhimu ya kujenga thamani ya mustakabali wetu. Tutatumia fursa zilizopo kwa kutafuta washirika na maeneo mapya ya ubia yanayojenge uwezo na kuauni njia za ziada za kukua kibiashara.

3. Kuisimamia Biashara Kama Mali ya Thamani
Mtaji ni rasilimali adimu hivyo tunapaswa kuitumia kwa busara. Ni lazima tuhakikishe kuwa mikakati yetu ya kuwekeza mitaji inahuisha fursa zitakazoongeza tija zaidi popote pale ilipo biashara yetu, Wakati huo huo, hatuna budi kuzifanyia kazi rasilimali zetu kwa kiwango cha juu kabisa, kuuza rasilimali zisizokuwa na faida ili kuhakikisha tunafufua migodi iliyokaribia kikomo cha umri kwa kuipa fursa mpya za kukua.

4. Kupanua Wigo
Tunapaswa kusimamia mapato na gharama ili kuhakikisha upatikanaji na udhibiti wa faida kutokana na mzunguko wa bei. Tunajenga mtizamo mpya wa kibiashara kuhakikisha kupanuka kwa wigo wa faida na kuendelea kuzalisha kwa kiwango cha ubora wa juu katika mchakato wetu mzima ili kuboresha na kundeleza thamani.

5. Kuwa na Matokeo Endelevu
Tutasimamia usalama na afya kama tunu yetu muhimu, ili kuonyesha adhma yetu kwa watu na usalama wao. Tunayo majukumu muhimu ya kulinda na kutunza mazingira na mahusiano mema kijamii, kitaasisi na kisiasa ili kuleta matokeo yaliyo ya manufaa kwa kila mmoja wetu.